JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI

MRADI WA USIMAMIZI WA TAKA NGUMU

TAARIFA YA USHIRIKISHAJI JAMII NA WADAU HADI MACHI, 2020

YALIYOMO

1. UTANGULIZI 1

1.1 MAELEZO YA MRADI 1

1.2 USHIRIKISHAJI JAMII 1

2. MALENGO NA DHUMUNI LA USHIRIKISHAJI JAMII 2

3. UTAMBUZI WA JAMII NA WADAU 2

4. MBINU ZA USHIRIKISHAJI JAMII NA WADAU 7

4.1 Mikutano na wadu wanaonufaika au wanaothirika na mradi 7

HITIMISHO 7

1. UTANGULIZI

1.1 MAELEZO YA MRADI

Kusudi la mradi unaopendekezwa ni mpango wa kubadilisha utaratibu wa usimamizi wa uzoaji wa taka ngumu kutoka utaratibu wa sasa ambapo Halmashauri ndiyo inayosimamia zoezi zima la usimamizi wa usafi na udhibiti wa taka ngumu na kwenda kwenye mfumo wa kuingia UBIA kati ya Serikali na Sekta binafsi.

Lengo kuu la mabadiliko haya ni kuboresha na kuongeza ufanisi katika huduma za uzoaji taka ili kuboresha Afya, Mazingira na ustawi wa Jamii ya wakazi wa Mtwara.

Hivyo timu ya uwekezaji kwa njia ya Ubia ya Halmashauri ilifanya zoezi la kuchukua maoni mbalimbali ya wadau wa maendeleo wanaoguswa moja kwa moja au wanaoguswa kivingine katika shughuli nzima za uzalishaji, uzoaji, uteketezaji na matumizi ya takangumu katika kata mbalimbali za Halmashauri.

1.2 USHIRIKISHAJI JAMII

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani inatumia mpango wa ushirikishaji wa jamii kwa kuwapa wadau fursa ya kushiriki kwa kutoa maoni juu mradi unaopendekezwa kuanzishwa. Ushirikishaji wa jamii ni hatua mojawapo inayotumika wakati wa Awamu ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi ili jamii ipate nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu mradi unaopendekezwa.

Ushiriki wa jamii utahusisha wadau mbali mbali wa jamii, wadau wote wanaoguswa moja kwa moja na wale wasioguswa moja na mradi watapata nafasi ya kuweza kushiriki katika katika kutoa maoni, ushauri au kero juu ya mradi unaopendekezwa kuanzishwa

2. MALENGO NA DHUMUNI LA USHIRIKISHAJI JAMII

Malengo ya ushiriki kwa awamu ya uwezekano wa Mradi ni:

- Kuijengea uelewa jamii kuhusu mradi pendekezwa ili jamii iweze kuumiliki mradi huo na kusaidia katika kutatua changamaoto mbalimbali zitakazojitokeza katika kipindi cha ujenzi na utekelezaji wa mradi
- Kuhakikisha jamii inapata uelewa wa Mradi uliopendekezwa na kupata nafasi ya kutoa maoni yao juu ya upembuzi wa awali wa mradi na baadaye kuboresha upembuzi mkuu wa mradi
- Kusaidia kupata maoni ya jamii kuhusu utayari wakulipia viwango vya ada na tozo mbalimbali za taka ngumu mbalimbali zinazotarajiwa kutozwa kwenye Kituo na maoni haya yatatumika katika kuandaa upembuzi yakinifu wa mradi.

3. UTAMBUZI WA JAMII NA WADAU

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikidani ilishirikisha wadau wafuatao ili kupata maoni yao juu ya mradi huu.

Ifuatayo ni orodha ya wadau walioshirikishwa ambao ni wanufaika wa moja kwa moja na wale ambao hawanufaiki moja kwa moja na mradi wa Usimamizi wa taka ngumu utakaoendeshwa kwa mfumo wa Ubia (PPP)

a. Taasisi

Jina	Aina ya Mdau	Uhusiano na mradi	Mchango	Majibu
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	Msimamizi wa shughuli za serikali	Mtoa huduma na mzalishaji wa taka	▪ Kuwe na utaratibu na ratiba maalumu za uzoaji taka katika maeneo yote ya halmashauri. ▪ Kuweke mpango mkakati wa kimazingira wa halmashauri ili kufanikisha kufikia hatua ya jiji.	Ushauri ulizangatiwa
Wamiliki wa Hotel	Matumizi	Mtoa Huduma na mzalishaji wa Taka	▪ Viwango vya tozo na ada zilizopendekewa ni rafiki kwao na kama mradi utawezesha kuboreshwa kwa huduma ▪	Ushauri ulizangatiwa
Mamlaka ya Bandari Mtwara	Matumizi	Mtoa Huduma na mzalishaji wa Taka	▪ Mradi huu utaleta ufanisi katika usimamizi wa taka ▪ Mtoa huduma afanye uboreshajii wa huduma kwa kuleta vifaa vya kisasa vitakavyoweza kutoa huduma katika meli zinazotia nanga kwenye bandari	Ushauri ulizangatiwa
Benki kuu ya Tanzania tawi la Mtwara	Matumizi	Mtoa Huduma na mzalishaji wa Taka	▪ Mtoa huduma atakaepewa kazi hiyo aweza kutoa huduma kwa ufanisi na kwa wakati ▪ Viwango vya tozo ni rafiki kwa watumiaji, lakini huduma iboreshwe ili mtumiaji atakapotoa ada ya taka iendane na ada aliyotozwa	Ushauri ulizangatiwa

Jina	Aina ya Mdau	Uhusiano na mradi	Mchango	Majibu
Chuo cha Stella Maris Mtwara	Matumizi	Mtoa Huduma na mzalishaji wa Taka	▪ Mradi utakuwa na manufaa kwa watumiaji kwa kuwa utaleta ufanisi katika huduma lakini pia huduma kutolewa kwa wakati	Ushauri ulizangatiwa
Wafanya bishara sokoni	Matumizi	Mtoa Huduma na mzalishaji wa Taka	▪ Viwango vitakavyotozwa na watakao kuwa wanatoa huduma hiyo, viendane na huduma bora itakayokuwa ikitolewa ▪ Mradi utakuwa na manufaa kama mtoa huduma ataweka vitendea kazi vya kutosha hasa vikusanyia taka katika maeneo tofautitofauti ya soko ili wateja waweze kutupa taka katika maeneo hayo na hivyo kupunguza uchafuzi wa mazingira	Ushauri ulizangatiwa
CBOs	Watoa Huduma	Wadau wa kutoa huduma uzoaji wa taka ngumu	▪ Halmashauri ihakikishe inasimamia vizuri endapo suala la UBIA litaingia kwenye shughuli za usafi na udhibiti wa taka ngumu. ▪ Mkandarasi atumie nguvu kazi /rasilimali watu wazoefu ambao wapo kwenye shughuli hizo kama kipaumbele cha ajira yaani waliokua wanashughulika na shughuli hizo.	Ushauri ulizangatiwa

Jina	Aina ya Mdau	Uhusiano na mradi	Mchango	Majibu
			▪ Kipato na vitendea kazi viwe vya kukidhi mahitaji ili kuongeza ufanisi katika kazi. ▪ Ajira zisiangalie umri bali uzoefu wa kazi na uwajibikaji. ▪ Pia walishauri ukusanyaji wa mapato uwe wa uhakika na wenye kufuata sheria na taratibu ziizowekwa na serikali na hatua za kisheria zichukuliwe kwa atakaye kiuka ▪ Mtoa huduma atakayepata zabuni ya kutoa huduma ya uzoaji wa taka ngumu kuwapatia nafasi vikundi vya uzoaji wa taka kuwa sehem ya mradi kwa kuwapa ajira au kuwa sehem mradi huo ▪ Mradi utawawezesha kupata ujuzi kutoka katika kampuni itakayokuwa inafanya kazi ya kutoa huduma	
Wananchi kutoka katika kata 18	Matumizi	Wazalishaji wa taka	▪ Halmashauri ihakikishe inasimamia vizuri endapo suala la UBIA litaingia kwenye shughuli za usafi na udhibiti wa taka ngumu. ▪ Gharama ya huduma ngazi ya kaya iwe kati ya Tsh 2000-2500 kwa mwezi, ▪ Taka zitolewe kwa wakati na kwa	Ushauri ulizangatiwa

Jina	Aina ya Mdau	Uhusiano na mradi	Mchango	Majibu
			ratiba maalumu iliyopangwa. ▪ Vituo vya kukusanyia taka viwe vya kutosha na vinavyotambulika ▪ Magari ya kusafirishia taka yaongezwe kwani kwa sasa hayatoshi ▪ Mkandarasi huyo afike hadi maeneo ambayo hayana vikundi wala kupitiwa na magari ya halmashauri	
Wachakataji wa taka (Recycler)	Matumizi	Mtumiaji wa taka ngumu kuzalisha malighafi	▪ Mbia atakapoanza kazi asikataze shughuli za uchambuzi na uokotaji wa taka eneo la dampo na sehemu za makusanyo. ▪ Itawarahishia kazi kwani taka zitatengwa kwa utaratibu mzuri hivyo kiwango chao cha kupata malighafi kitaongezeka. ▪ Kuwe na eneo maalumu la kupata malighafi zao hata kama ni kwa kugharimia kwani uwepo wa mbia kutarahisisha upatikanaji wa malighafi hizo.	Ushauri ulizangatiwa

4. MBINU ZA USHIRIKISHAJI JAMII NA WADAU

Mbinu mbalimbali zilitumika katika kushirikisha wadau ili kupata maoni na ushari juu ya mradi pendekezwa

4.1 Mikutano na wadu wanaonufaika au wanaothirika na mradi

Halmashauri ya manispaa ya Mtwara-Mikindani ilifanya mikutano mbalimbali na wadau ambao ni wanufaika au waathirika wa mradi. Mikutano ilifanyika na kukutana na wadau kulingana na uhusika wa mdau katika mradi pendekezwa

HITIMISHO

Ushirikishaji jamii ni dhana chanya inayokusudia kuleta upokeaji na utumiaji mzuri wa mradi ili kuepuka migogoro isiyokua ya lazima katika uendeshaji wa mradi. Timu ya usimamizi wa mradi inasimamia na itaendelea kusimamia ushirikishaji wananchi katika kupokea maoni/mapendekezo na kuyafanyia kazi.

Mratibu wa mradi
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKIDANI

Kwa maoni au ushauri wasiliana nasi kwa namba zifuatazo

Simu na. 0674 080 394
0787 027 877
0712 846 794
0717 036 200
Barua pepe: johnandrew642@gmail.com
gasperjosephat@yahoo.com